MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA
JARIDA LA HALI YA HEWA


**Na: 30. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Julai 11-20, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Julai 21-31, 2019**

**Muhtasari**

- Hali ya baridi inayotarajiwa katika maeneo ya miinuko inaweza kuathiri ukuaji na kukomaa kwa mazao mashambani
- Hali ya ukavu inayotarajiwa itafaa kwa uvunaji,ukaushaji na uhifadhi wa mazao.
- Wakulima wanashauliwa kutunza chakukula cha ziada kuepuka upungufu wa chakula unaoweza jitokeza.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2019

Katika siku kumi za dikadi, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika zaidi hivyo kuimarisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kupungua nguvu na kuruhusu ukanda wa mvua kuwa kaskazini mwa ziwa Victoria. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilikua katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi wakati upande wa kaskazini magharibi (karibu na pwani ya Somalia) joto lilikuwa chini ya wastani na kusababisha mkondo wa mgandamizo mdogo wa hewa kuwa katika maeneo ya ziwa Victoria. Aidha, hali hiyo ilisababisha upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki kuelekea katika ukanda wa pwani. Upande mwingine joto la bahari la juu ya wastani hadi wastani kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki liliendelea kuwepo. Hii iliendelea kupunguza nguvu ya upepo wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Kongo kuelekea katika maeneo ya magharibi na ukanda wa ziwa Viktoria katika nchi ya Tanzania. Kuendelea kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia kulisababisha kujitokeza kwa vipindi vya upepo mkali na baridi katika maeneo mengi ya nchi.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Julai 11- 20, 2019

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2019

Kwa kipindi hicho maeneo mengi ya nchi yalikua makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini magharibi hususan mkoa wa Mara ambayo yamepata mvua za nje ya msimu. Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya 26 mm na 50 mm kama inavyojionesha katika kielelezo.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2019

Hali ya ukavu iliyojitokeza katika kipindi hiki cha dikadi ilisaidia shughuli za uvunaji ,ukaushaji na uhifadhi wa mazao. Maeneo machache yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hususan katika mkoa wa Mbeya,Iringa ,Kigoma na Dodoma uvunaji wa zao la mahindi ulikuwa ukiendelea. Maeneo ya mikoa ya kusini hususan Mtwara na Lindi upuliziaji wa madawa ya kuulia wadudu waharibifu wa zao la Korosho uliendelea. Maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka wakulima walijihusisha zaidi na shughuli za uvunaji,ukaushaji na uhifadhi. Kwa baadhi ya maeneo machache ya mkoa wa Mara wakulima walijihusisha na uvunaji wa maharage.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2019

Kina cha maji kwenye mabwawa na mitililiko ya maji kwenye mito viliendelea kupungua kiasi kwa maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu inayoendelea kupungua kutokana na hali ya ukavu na upepo.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 21-31, 2019

Katika siku kumi za dikadi, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika zaidi hivyo kuimarisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia kuendelea kupungua nguvu hivyo kuendelea kuruhusu ukanda wa mvua kuwa Kaskazini mwa ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi wakati upande wa kaskazini magharibi (karibu na pwani ya Somalia) joto linatarajiwa kuwa chini ya wastani, hivyo kusababisha mkondo wa mgandamizo mdogo wa hewa kuwa katika maeneo ya ziwa Viktoria. Aidha, hali hiyo itasababisha upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki kuelekea katika ukanda wa pwani. Kuendelea kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia kunatarajiwa kusababisha kujitokeza vipindi vya upepo mkali na baridi katika maeneo mengi ya nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 21-31, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata mvua na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) , kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) , nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) , kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na mawingu kiasi.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 21-31,2019

Hali ya mvua inayotarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa ziwa Viktoria inaweza kuathiri mazao yaliyokomaa ambayo mashambani.Wakulima wanashauriwa kuchukua tahadhari kuepusha uharibifu wa mazao. Hali ya ukavu inayotarajiwa kwa maeneo mengine ya nchi itasaidia ukaushaji na utunzaji wa mazao na inaweza sababisha kupungua kwa maji na malisho ya mifugo.Pia hali ya baridi inayotarajiwa katika maeneo ya miinuko inaweza kuathiri ukuaji na kukomaa kwa mazao mashambani. Wafugaji wanashauriwa kutumia vizuri maji na malisho yaliyopo. Wakulima pia wanashauriwa kutunza chakula cha ziada kuepuka upungufu wa chakula hususan maeneo ambayo shughuli za uvunaji zimemalizika. Wakulima ,wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maafisa ugani katika maeneo yao kwa ushauri zaidi .

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 21-31, 2019

Kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na kuendelea kwa hali ya ukavu,mvukizo na upepo. Watumiaji wa maji wanashauriwa kutumia vizuri maji yaliyopo.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***